Jumiko la Maliasili Tanzania

Tanzania Natural Resource Forum

*HABARI JUU YA WANYAMAPORI KATIKA TANZANIA*

**Wanyamapori kwa watanzania wote: Kusimamisha upotevu, kuendeleza raslimali na kupanua mafao**

# CHAPISHO NA. 1

## MWISHO WA WANYAMA? KUPUNGUA NA KUHARIBIWA KWA WANYAMAPORI TANZANIA

**MASUALA MUHIMU:**

**⇨ Takwimu bora na za kisasa zinapendekeza kuwa wanyamapori wanapungua katika maeneo yote muhimu ya wanyamapori na mifumo ya uhifadhi Tanzania, ikiwa ni pamoja na maeneo makubwa yaliyohifadhiwa kama vile Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba.**

*Kwa kushirikiana na*

*© JMT 2008*

## Tanzania ina maeneo makubwa na wanyama wengi duniani

Tanzania ina idadi kubwa ya wanyama wakubwa waliobaki kupita taifa lolote lile duniani. Tanzania ndiyo yenye idadi kubwa kabisa ya simba na nyati wengi zaidi. Na idadi ya tembo inayoongezeka inakaribiana na ile ya Botswana ambayo ina idadi kubwa Barani Afrika. Makundi ya wanyamapori katika mifumo ya ikolojia ya Serengeti – zaidi ya pundamilia milioni mbili, nyumbu, na jamii ya swala – yamkini inawakilisha mkusanyiko mkubwa wa wanyamapori waliobaki katika sayari yetu. Tanzania imeanzisha moja ya mitandao mikubwa ya maeneo yaliyohifadhiwa kuliko nchi yoyote ile duniani, takribani asilimia 30 ya eneo la nchi limehifadhiwa kama Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Misitu ya Hifadhi.

Idadi ya wanyamapori Tanzania imetawanyika wakipatikana ndani ya hifadhi, mapori ya akiba na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa mahali ambako wanaishi na binadamu katika ardhi za vijiji na za watu binafsi. Wanyamapori ni msingi wa biashara ya utalii wa kupiga picha na ya uwindaji na hivyo, ni raslimali muhimu ya kiuchumi Tanzania.



*Uhamaji wa nyumbu Serengeti – tukio kubwa duniani*

## Maeneo ya wanyamapori

Wanyamapori Tanzania husimamiwa chini ya mifumo ya kiasasi tofauti. Kila mfumo una malengo yake na changamoto za kiuhifadhi. Muhtasari unafuata chini:

| Aina & Malengo | Msimamizi | Asilimia ya eneo la nchi |
|---|---|---|
| Hifadhi za Taifa<br>*Ulinzi na matumizi yasiyo ya uvunaji tu* | Serikali<br>(Shirika la Umma) | *4.4%* |
| Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro<br>*Ulinzi pamoja na matumizi mseto ya ardhi bila uvunaji* | Serikali<br>(Shirika la Umma) | *0.9%* |
| Mapori ya Akiba<br>*Ulinzi pamoja na uvunaji na matumizi yasiyo ya uvunaji ya wanyamapori (Uwindaji na kupiga picha)* | Serikali<br>*(Idara ya Wanyamapori)* | *13.0%* |
| Mapori Tengefu<br>*Uvunaji na matumizi yasiyo ya uvunaji ya wanyamapori (Uwindaji na kupiga picha)* | Serikali<br>*(Idara ya Wanyamapori pamoja na Halmashauri za Wilaya)*<br>*(Mapori Tengefu mara nyingi hubebana na Ardhi za Vijiji)* | *5.5%* |
| Maeneo ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Jamii (WMA)<br>*Uvunaji na matumizi yasiyo ya uvunaji ya wanyamapori (Uwindaji na kupiga picha)* | Asasi zilizoidhinishwa za WMA kwa niaba ya Halmashauri za Vijiji (kwa kushirikiana na vijiji wanachama, Serikali za Mitaa na Idara ya Wanyamapori) | *3.7%* |
| Misitu ya Hifadhi<br>*Ulinzi pamoja na matumizi ya uvunaji* | Idara ya Misitu na Nyuki na Halmashauri za Wilaya | *16.2%* |
| Misitu ya Vijiji<br>*Uvunaji na matumizi yasiyo ya uvunaji wa mazao ya misitu na ya wanyamapori* | Serikali za vijiji kwa niaba ya Halmashauri za Vijiji | *2.6%* |

*Muhimu: Misitu ya Vijiji imeongezewa katika takwimu hizi kwa kuwa Misitu ni muhimu kwa ajili ya wanyamapori hasa kwa kuzingatia bioanuai isiyopatikana kokote duniani. (Takwimu zimetolewa katika vyanzo tofauti na maeneo mengine yanaingiliana)*

## Tanzania inapoteza wanyamapori

Licha ya maeneo makubwa yaliyohifadhiwa na mengine yenye wanyamapori yanayochukua karibu asilimia 40 ya eneo la nchi, takwimu za kiutafiti za hivi karibuni zilizoandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) na kuchapishwa katika majarida ya kimataifa ya kisayansi zinaonesha wazi kuwa aina kiasi na mtawanyiko wa wanyamapori Tanzania unaendelea kupungua kwa kasi.

Takwimu hizi zina msingi katika hesabu za wanyama zilizofanywa toka angani katika maeneo muhimu ya wanyamapori Tanzania – ikiwa ni pamoja na maeneo yaliyohifadhiwa na maeneo ya vijiji yanayozunguka maeneo yaliyohifadhiwa. Na takwimu katika hesabu hizo zimekusanywa tangu mwishoni wa miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000. Hivyo takwimu zinaonesha ni kwa vipi na wapi wanyamapori wamepungua au kuongezeka kwa kipindi cha miaka kumi.



*Hesabu ya wanyama iliofanyika kwa ndege katika mfumo ikolojia wa Tarangire*

***Takwimu katika Kielelezo Na. 1 zinadhihirisha maeneo yote muhimu ya wanyamapori, aina ya wanyama wanapungua kwa uwingi kuliko kuongezeka.***

*Na zaidi:*

- ⇨ Idadi ya wanyama wakati wa kiangazi katika mfumo ikolojia wa Ruaha Mkuu inaashiria kuwa karibu asilimia 73 ya spishi zimepungua sana. Na ni karibu asilimia 9 tu ya spishi ndiyo zimeongezeka kwa kiwango kizuri.
- ⇨ Katika mfumo ikolojia wa Tarangire asilimia 46 ya spishi zimeonesha kupungua wakati wa hesebu za kiangazi kukiwa hakuna spishi iliyoongezeka. Wakati wa hesabu za masika asilimia 68 ya spishi zilipungua na asilimia 7 tu ya spishi ziliongezeka.

*Kielelezo Na. 1: Asilimia ya wanyamapori wanaopungua na asilimia ya wanyamapori wanaoongezeka katika maeneo tofauti ya kijiografia Tanzania kwa kufuata takwimu za hesabu za angani (kipindi cha masika) mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 2000.*




*Muhimu: Kupungua kwa spishi kumeoneshwa kwa rangi nyekundu na spishi zilizoongezeka kwa rangi ya kijani. Kielelezo hiki kinaonesha tu kitakwimu kiasi muhimu na kilichopungua na kuongezeka. Na hiyo ndiyo sababu hesabu yake katika kielelezo haitimii asilimia 100.*

***Kuendelea kupungua kwa idadi ya wanyamapori katika mifumo ikolojia muhimu nchini kutakuwa na athari kubwa za kiuchumi kitaifa.***

Mfumo ikolojia wa Tarangire (ukijumuisha Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Ardhi za Vijiji vinavyoizunguka) ni kitu muhimu katika utalii kaskazini mwa Tanzania, na Ruaha ni Hifadhi ya Taifa kubwa katika Afrika, ambayo inapatikana katika eneo la kusini linalokua kwa kasi kiutalii.

Asilimia kubwa ya spishi zilipungua katika eneo lililohesabiwa la Burigi-Biharamulo, ambako asilimia 69 ya spishi zilipungua wakati wa hesabu za masika na asilimia 80 zilipungua wakati wa hesabu za kiangazi. Hakuna spishi iliongezeka katika misimu yote. Katika Burigi-Biharamulo, upungufu huu wa kutisha kwa muda unaweza kuhusishwa na wakimbizi katika eneo hilo kutokea Rwanda katikati ya miaka ya 1990 na waliovuna wanyamapori bila kudhibitiwa. Kielelezo Na. 2 kinaonesha spishi zilizochaguliwa ambazo zinapungua na kuongezeka katika kipindi cha kuidadi

*Kielelezo Na. 2: Asilimia ya maeneo yaliyohesabiwa ambako spishi za wanyama wakubwa zimepungua na kuongezeka mwishoni mwa miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000.*




*Muhimu: Kupungua kwa spishi kumeoneshwa kwa rangi nyekundu na spishi zilizoongezeka kwa rangi ya kijani. Spishi zilizohesabiwa ni pundamilia, nyumbu, palahala weusi, palahala hudhurungi, korongo, twiga, tembo, pofu na mbogo.*

**Si tu idadi ya wanyamapori inapungua katika maeneo muhimu ya wanyamapori lakini spishi nyingi za wanyama wakubwa zinapungua kwa uwingi.**

wanyamapori kwa miaka kumi. Kwa ujumla, kwa mujibu wa takwimu hizi, wanyama jamii ya swala na pundamilia walipungua.

Mathalani:

- ⇨ Pundamilia ambao ni spishi iliyo na wanyama wengi waliotawanyika na kusambaa katika maeneo mengi Tanzania wamepungua katika asilimia 80 ya kanda zilizokaguliwa wakati wa masika na kiangazi. Hakukuwa na rekodi ya ongezeko la pundamilia mahali popote. Hii inaonesha kuwa pundamilia wanapungua sana kote Tanzania.
- ⇨ Spishi nyingine za jamii ya swala kama vile palahala mweusi ni muhimu kwa uwindaji wa kiutalii. Spishi hizi nazo zinapungua. Takwimu zinaonesha kuwa palahala weusi wamepungua katika nusu ya maeneo yaliyokaguliwa na hakuna mahali walipoongezeka. Palahala hudhurungi walipungua katika hesabu za masika na kiangazi.
- ⇨ Twiga wameonesha kutobadilika wakati tembo wameongezeka katika maeneo mengi yaliyokaguliwa. Sababu za kuongezeka kwa tembo ni kwamba kuidadi kulipoanza mwisho mwa miaka ya 1980 tembo walikuwa katika zahama ya kuwindwa na majangili kwa ajili ya nyara zao. Kufuatia kuzuiwa kwa biashara ya meno ya tembo na uboreshwaji katika usimamizi wa sheria kuanzia 1989 na kuendelea idadi ya tembo ikarejea.

Chapisho Na. 2 huonesha mchanganuo wa kiini cha visababishi.

**Takwimu bora za kisayansi zinaonesha kupungua kwa wanyamapori katika maeneo yote ya muhimu ya wanyama na mifumo ikolojia yakiwemo maeneo nyeti yaliyohifadhiwa kama vile Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba.**

**Vilevile takwimu zinaonesha spishi nyingi ukiondoa tu twiga na tembo wamepungua kwa kasi kwa idadi zao tangu katikati ya miaka ya 1980.**

*Chapisho hili lina msingi katika muhtasari wa takwimu zilizochaguliwa kutoka: Stoner, C.,T. Caro, S. Mduma, C. Mlingwa, G. Sabuni, M. Borner, and C. Schelten. 2007. Changes in large herbivore populations across large areas of Tanzania. African Journal of Ecology 45: 202-215.*